MWONGOZO KWA WANAOANZA KUWEKEZA KATIKA MASOKO YA MITAJI

1.0 Utaratibu

Je, wewe una nia ya kushiriki katika soko la mtaji lakini haujui uanze vipi? Ufuatao ni mwongozo sahihi:

1.1 Hatua ya kwanza: Fanya tathmini ya kibinafsi kuhusu fedha

Chunguza madhumuni yako ya kifedha, mapato yako, matatizo na jinsi unavyoweza kuhimili hasara. Jiulize iwapo uko tayari kifedha kuwekeza katika soko la mtaji? Kwa wanaoanza si vizuri kukopa ili kuwekeza katika masoko ya mitaji. Katika soko ambalo linayumbayumba, unaweza kupoteza pesa ulizokopa na ilhali sharti ulipe mkopo uliokopa.

1.2 Hatua ya pili: Fanya biashara na kampuni silizosajiliwa pekee

Tafuta mshauri wako kuhusu maswala ya uwekezaji wa fedha na ufungue akaunti nao. Mshauri wako, awe ni benki ya uwekezaji, dalai au kampuni nyingine yoyote inayokushauri kuhusu uwekezaji sharti awe na kibali kutoka kwa Halmashauri ya Masoko ya Mitaji (CMA). Kwa maelezo zaidi, tambelea mtandao wetu internet www.cma.or.ke au piga simu 221910.

1.3 Hatua ya tatu: Fungua akaunti ya Central Depository System (CDS)

Central Depositry System ni utaratibu wa tarakilishi unaoendeshwa na campuni iitwayo Central Depository and Settlement Corporation (DCSC) ambao huwezesha kuhifadhiwa kwa amana katika akaunti za kilektroniki zilizo funguliwa na wenye hisa. CDSC Husimamia ulipaji wa mahitaji yote ya kifedha kupitia Soko la Hisa la Nairobi (hisa na hati fungani) kwa haraka na ulinzi mkali.

Unafungua akaunti ya CDS kwa kujaza na kutia sahihi akaunti ya amana katika fomu ya kufuungua kupitia ajenti wako, kwa kupeana picha mbili za pasipoti na nakala ya kitambulisho chako cha kitaifa. CDA ni ajenti; awe dalali, benki ya uwekezaji au mdhamini wa benki, ambaye ameruhusiwa na Central Depository and Settlement Corporation kufungua akaunti za CDS kwa niaba ya wawekezaji.

1.4 Hatua ya nne: Chukua udhabiti wa akaunti yako ya biashara

Hakikisha umesimamia ipasavyo akaunti yako ya biashara katika benki yako ya uwekezaji au dalali. Akaunti hizi ni za matumizi yako pekee. Usimkubali yeyote, akiwemo mwakilishi wako kutumia akaunti yako kwa kufanya biashara. Ni akaunti hii ambayo utakuwa ukiirejelea, na kujua ni biashara gani imefanywa na benki ya uwekezaji au dalai, kwa niaba yako. Ni muhimu kuhakikisha kuwa unapata stakabadhi zote muhimu kwa biashara yako ikiwa ni pamoja na risiti, taarifa ya biashara, mikataba ya uuzaji na ununuzi, taarifa za akaunti ya CDS, mgao na kadhalika. Una haki ya kutoa malalamiko iwapo biashara ambayo haujaidhinisha imefanywa kwa akaunti yako.

2.0 Ushauri wa kuwekeza ufaao katika masoko ya mtaji

Haya ni baadhi ya mambo ya kimsingi mwekezaji yeyote yule anahitajika kuyajua anapoingia katika uwanja wa kuwekeza katika masoko ya mitaji kwa jumla na katika soko la hisa :



2.1 Jua aina za bidhaa za uwekezaji zilizopo

Soko la mtaji la Kenya linatoa bidhaa za uwekezaji zifuatazo:
- Hisa (Shares)
- Hatifungani (Bonds)
- Uwekezaji wa kijumla (Collective Investment Schemes)

2.2 Jua hali ya uwekezaji wako

Mwekezaji mwerevu huchagua mmoja au zaidi ya rasilmali za uwekezaji zilizotajwa hapo juu sio tu kulingana na malengo yake na kiwango cha fedha kilichopo, bali pia kulingana na uwezo wako wa kuhimili dhima. Kila uwekezaji huwa na dhima; nyingine huwa na dhima nyingi kuliko nyingine. Unahitajika kuchunguza iwapo wewe ni mtu anayeweza kustahamili dhima au ni mtu anayeogopa dhima, ili uweze kufuatilia mpango wa uwekezaji ulio wa kasi, kadri au unaozingatia uhifadhina. Kwa maneno mengine, mkakati wa uwekezaji unaozingatia hali yako ya dhima, kwani unapaswa kufurahia uchaguzi wako. Iwapo, kwa mfano, dhima yako ni ya kiwango cha chini, basi malengo yako yanapaswa kuwa chini upande wa uwekezaji hisa, na juu kwa upande wa hatifungani na uwekezaji wa kijumla

2.3 Chagua bidhaa ifaayo ya uwekezaji

Hatifungani ni ala za soko la mitaji zinazowavutia wawekezaji wa taasisi, na huhitaji kiwango cha shilingi 50,000 ili kuendesha biashara.

Wewe kama mwekezaji wa rejareja, itakuwa bora kwanza kufanya biashara kwa uwekezaji hisa, na uwekezaji wa kijumla. Lakini utachagua gani?

Iwapo wewe hutumia muda mwingi kutafiti kuhusu hisa, na hali ya soko la hisa na hufurahia dhima ya juu inayoambatana na mazao ya juu, basi uwekezaji wa mtaji wa moja kwa moja katika soko la hisa huenda ukakufaa.. Iwapo, kwa upande mwingine, unahitaji kuondolewa uchovu wa kila siku wa kushughulikia uwekezaji wa moja kwa moja, basi huenda ukahitajika kuwekeza katika uwekezaji wa kijumla.

Utaratibu ambao mtu hufuata katika masoko ya mtaji hutegemea malengo ya uwezekaji ikiwa ni pamoja na:

1.

- Kuwa na biashara iliyo na faida kiasi.
- Mapato ya kifedha (tafuta kampuni ambazo hupeana bakshishi na zile zenye uwezo wa kuongeza bei).
- Kuwa na fedha mgao mara kwa mara (tafuta kampuni zilizo na hatifungani za muda mrefu).
- Nia ya kuchukua umiliki wa kampuni (mtu atahitajika kuwaalifu wenye kampuni nia yako yakufanya hivyo baada ya kumiliki asilimia fulani ya kampuni).
- Kuwa na iyo hadhi ya kwamba wewe unamiliki kampuni fulani.

2.4 Fanya utafiti kabla ya kuwekeza

Usiwekeze pesa zako vyovyote vile hadi umeelewa habari zote muhimu kuhusu uwekezaji unaodhamilia.

Kwa hisa na hatifungani, inamaanisha kuchagua amana zako kulingana na misingi bora ya kampuni inayohusika, kuliko maelezo mapya motomoto ya watafiti. Jitayarishe mwenyewe kufanya (au mwulize dalali wako au benki yako ya uwezekaji kufanya) uchunguzi wa kina wa kuchambua ripoti za kila mwaka za kampuni, akaunti na taarifa nyingine huku ukizingatia yale yanayotendeka katika sekta tofauti, nchini na kwingineko katika nyanja ya uwezekaji. Unaweza kutakmini kujumuisha uchunguzi wa misingi bora ya kampuni unayotaka kuwekeza pamoja na kuchunguza kwa makini ni wakati gain mwafaka wa kuingia kwenye soko la hisa. Ni vizuri kuchunguza mapendekezo ya marafiki au uvumi wowote juu ya hisa au hatifungani, hasa iwapo huwawezi kukuelezea hayo mapendekezo kinaga naga mpaka uelewe. Sheria muhimu katika ununuzi wa hisa na hatifungani ni kwamba mnunuzi sharti awe macho (makini).

Kwa mipango ya Uwekezaji wa kijumla (Collective Investment Schemes) inamaanisha kuchunguza kwa makini hazina ya mipango hiyo pamoja na kampuni inayosimamia huo mpango kabla ya kuwekeza. Inafaa kusoma na kuelewa maelezo ya hazina hiyo, hati ya amana, ripoti za kifedha, malengo yake ya uwekezaji and dhima zinazohushiswa. Fanya utafiti wako, huku ukichunguza utendaji kazi wa hazina ya kampuni kwa kipindi fulani ikilinganishwa na hazina nyingine. Lakini hata hivyo kumbuka kuwa rekodi ya hazina sio hakikisho kamili kuwa itafanya vizuri siku za usoni.

Kwa hatifungani, unahitajika kuchunguza mwelekeo wa viwango vya riba. Ingawa mwekezaji hawezi kupoteza kiwango cha kwanza cha uwekezaji katika amana, thamani inaweza kupungua kutokana na mfumuko wa bei huku ushindani wa amana hizo ukipungua bei kwa sababu ya kupanda kwa viwango vya riba katika uchumi huo.

2.5 Imarisha mapato yako ya kifedha kwanza

Usiingilie mpango wowote wa uwekezaji iwapo haujaimarisha mapato yako ya kifedha kukidhi mahitaji ya matumizi yako ya kati ya miezi 6 na 9 ili kusimamia dharura yoyote ya kifedha. Akiba kama hiyo ni muhimu kwani bila akiba itokeapo matatizo ya kifedha, unaweza kuanza kutoa pesa kutoka kwa mpango wako wa uwekezaji mapema kuliko inavyotakikana hivi kwamba utaahiri kasi ya huo mpango. Pia, lipa madeni ya muda mfupi kwanza kabla ya kutumia akiba yako katika uwekezaji. Sharti uelewe hatari kubwa iliyoko ya kuwekeza katika pesa za kukopa.

2.6 Wekeza ukifiria kupata faida baada ya muda

Kufikiria maswala ya muda mfupi kunaweza kutatiza mafanikio ya muda mrefu. Kumbuka kuwa katika uwekezaji wowote, sharti kutakuwepo na maswala ya muda mfupi ambayo huenda yakapita yale ya muda mrefu, kwa hivyo lazima uwe na uwezo wa kushikilia uwekezaji wako kwa muda mrefu. Historia inaonyesha kuwa masoko ya uwekezaji daima huwa na faida baada ya muda kidogo na huendelea na faida hatazaidi vile masiku yanavyo endelea. Lakini iwapo unataka kutuhumu na kupata faida ya haraka, fanya hivyo ukiwa macho na daima sio kwa pesa nyingi kuliko unavyoweza kuhimili kuzipoteza. Sheria sio tu kuwekeza na kukaa muda mrefu au kutuhumu kwa muda mfupi bali ni kuwekeza na kufanya uchunguzi. Ata unapowekeza na kukaa kwa muda mrefu inastahili kuchunguza nafasi zinazojitokeza mara kwa mara zakutengeneza pesa katika soko la hisa.

2.7 Usiweke mayai yako yote kwenye kapu moja

2.7.1 Njia iliyo bora ya kupunguza dhima huku ukichunguza viwango vya faida utakayopata ukiwa na uwekezaji wa aina mbalimbali. Iwapo hisa ndizo unazowekeza ni bora kuwekeza katika sekta mbalimbali, kama ni kwa mpango Uwekezaji wa kijumla (Collective Investment Schemes) ni mzuri kuwekeza kwa mipango tofauti. Hasara katika hazina moja inaweza kufidiwa nafaida kutoka kwa hazina nyingine.. Kama wasemavyo, kuna usalama katika idadi kubwa. Hata hivyo, usiwe na kampuni nyingi kupita kiasi. Kuwa na kampuni nyingi kupita kiasi kwa hazina yako kunaweza kupunguza faida yako.



2.8 Kaa imara

Chunguza na fuatilia uwekezaji wako kila mara ili kuhakikisha kuwa mpango wako wa uwekezaji bado unalingana na malengo yako ya kibiashara, chunguza bei, hudhuria mkutano wa kila mwaka ya kampuni ulizowekeza, soma nakala za utafiti. Fuatilia kwa makini uwekezaji wako kubainisha iwapo matarajio yako ya kifedha yametimika, au iwapo kuna mahitaji ya kupanga upya uwekezaji wako ikiwa rasilmali zako haziendi sawa. Usiogope kubadilisha uwekezaji mmoja na mwingine kama ni itaimarisha uwekezaji wako ukifanya hivyo.

2.9 Tahadhari na ulaghai

Habari ambazo zimetolewa hapa ni mwongozo tu. Iwapo una tashwishi, tafadhali wasiliana na Halmashauri ya Mtaji (CMA)nambari ya simu 221910 au Soko la Hisa la Nairobi (NSE) nambari ya simu 2306892.

MAELEZO YA BAADHI YA ISTILAHI AMBAZO HUTUMIKA MARA KWA MARA

Amana tendi (Active Securities)

Hizi ni amana ambazo hutumiwa sana kufanya biashara katika soko la hisa.

Kuchukua umiliki (Acquisition)

Haya ni makampuni yanayoshindana kibiashara (umiliki na usimamizi) yaliy-oletwa pamoja chini ya usimamizi mpya.

Maelezo ya kampuni (Articles of Association)

Hii ni stakabadhi inayoelezea malengo, mahali pa kufanyia kazi na maelezo ya kampuni

Ajenti (Agent)

Ajenti kwa kawaida ni mwakilishi wa dalali nahufanya biashara ya kununua na kuuza amana ili kupata kiwango fulani kutoka kwa dalali.

Yote au bila (All Or None-AON)

Hiki ni kizuizi kinachowekwa kwa agizo ili kuzingatia agizo lote wakati Fulani kwa jumla bila kuipunguza kwa viwango kadhaa.

Barua ya umiliki (Allotment Letter)

Hii ni stakabadhi inayotolewa na kampuni kwa wawekezaji kuonyesha hisa(amana)alizotengewa kila aliyetuma maombi ya amana kama hizo

Ripoti ya mwaka (Annual Report)

Hii ni stakabadhi inayotolewa kila mwaka na kampuni kwa wenye hisa ikionyesha taarifa ya mwenyekiti, na hali ya kifedha zikiwemo rasilimali,deni,faida na hasara na habari nyingine muhimu kuhusu kampuni. Kuchapisha ripoti ya mwaka ni sharti iliyowekewa kampuni zote za umma.

Mkutano wa kila mwaka (Annual General Meeting-AGM)

Huu ni mkutano wa lazima kwa mujibu wa sheria unaofanywa kila mwaka na kampuni zote za umma ambapo mwenyehisa hualikwa kuhudhuria ili kujadili maswala kadhaa na utendaji kazi wa kampuni yao.

Kuungana (Amalgamation)

Hii ni hali ya kampuni mbili ambazo hapo awali zilikuwa tofauti kuungana ili kuunda kampuni moja mpya.

Rasilimali (Assets)

Neno rasilimali inajumuisha mali yote na uwezekaji ikiwa ni pamoja na pesa taslimu, na pesa zilizowekwa kwenye benki ambazo kampuni inamiliki.

Amana zilizo kwenye deni (Asset-Backed Debt Securities-ABS)

Hizi ni amana za kibinafsi zilizo kwenye deni ambazo hutolewa baada ya mtu kuweka thamana.

Agizo ya bei iliyo bora zaidi (At Best Order)

Hii ni agizo kutoka kwa mteja kwa dalali wake akimwagiza dalali kutumia uamuzi wake katika kutekeleza agizo kwa bei iliyo bora zaidi.

Mfanyibiashara wa amana aliyeidhiniwa (Authorized Securities Dealer)

Hii ni benki iliyopewa kibali chini ya sheria ya benki au taasisi ya kifedha iliyoidhinishwa na Halmashauri ya CMA kushughulikia amana ziliozoorodheshwa katika kitengo cha amana kwenye soko la hisa.

Mtaji wa hisa ulioidhinishwa (Authorized Share Capital)

Huu ni mtaji wa hisa wa kampuni ambao umeelezewa katika maelezo ya kampuni kama inavyotakikana kisheria.Mtaji wa hisa ulioidhinishwa hutolewa kutegemea thamani ya hisa kwa idadi ya hisa zilizoidhinishwa. Ili kuongeza mtaji wa hisa, azimio sharti lipitishwe na idadi kubwa ya wenye hisa na maombi yatumwe kwa msajili wa makampuni.

Wasilisho baya (Bad Delivery)

Wasilisho la amana kuhusiana na biashara (awe kutoka kwa mteja hadi kwa dalali au kutoka kwa dalali hadi dalali mwingine) huchukuliwa kuwa "mbaya" iwapo kuna dosari katika cheti cha hisa au hati hamisho au iwapo haikuwakilishwa kwa wakati ufaao.

Mdhamini asiyekuwa na nia (Bare Trustee)

Huyu ni mdhamini asiyekuwa na nia ya kufaidika katika suala linaloshughulikiwa katika udhamini.

Mbahatisha hisa (Bear)

Mnunuzi wa jumla wa hisa anayeuza hisa zinapokuwa na bei ya juu na kutumaini kuwa zitateremka bei ili azinunue tena zikiwa bei ya chini.

Bei nukuzi (Bid)

Hii ni bei inayopendekezwa, ambayo ni bei ya juu mnunuzi yuko tayari kulipia ili kununua amana.

Nyongeza (Bonus)

Hizi ni hisa zaidi zinazotolewa kwa wenyehisa katika mgao maalum na kulipwa kutoka kwa akiba ya kawaida ya mapato ya kampuni.Hisa nyongeza mara nyingi hutolewa badala ya kulipa mgao wa faida, ingawa kampuni inaweza kutoa zote kwa wakati mmoja.

Hatifungani (Bonds)

Hizi ni dhamani za mkopaji zinazotolewa na serikali,shirika la taifa au kampuni, yenye riba isiyobadilika. Wenye hatifungani hupata riba hata kama mwenye kutoa riba hajatengeneza faida.

Mlanguzihisa (Bull)

Mtu anayenunua hisa kwa imani kuwa zitapanda bei na hivyo ataweza kuziuza kwa bei ya juu zaidi.

Faida ya kimtaji (Capital Gain)

Ni tofauti baina ya bei ya kununulia mali na bei ya kuziuza hapo baadaye, ambapo bei ya kuuzia ni kubwa kuliko ya kununulia.

Hasara ya kimtaji (Capital Loss)

Ni tofauti baina ya bei ya kununulia mali na bei ya kuziuza hapo baadaye, ambapo bei ya kuuzia ni kidogo kuliko ya kununulia.

Masoko ya mtaji (Capital Markets)

Hapa ni mahali ambapo mtu au shirika anaweza kupata mkopo wa muda mrefu kwa ajili ya kuendeleza viwanda au biashara hasa katika uwekezaji usioham-ashika. Masoko haya huwezesha kuweka akiba katika uwekezaji zalishi na kupata faida

Akiba ya mtaji (Capital Reserves)

Hii ni sehemu ya mapato ya kampuni ambayo kwa kawaida hayajagawa kama mgao nahujumuisha rasilimali na hisa. Inaweza kugawa kama hisa nyongeza kwa wenye hisa.

Central Depository Settlement Corporation (CDSC)

Ni kampuni iliyoidhiniwa na Halmashauri (CMA) kwa mujibu wa kifungu 5 cha sheria ya Central Depositories ili kuidhinisha utaratibu wa kuweka rubuni kwa minajili ya kushughulikia amana zote pamoja katika sehemu moja maalum.

Siku ya mwisho ya toleo (Closing Date Of Offer)

Hii ni siku ya mwisho ya kukubali pesa kutoka kwa wawekwzaji na kampuni inayoshajilisha amana kwa umma kwa minajili ya kusajiliwa katika soko la hisa.

Bei ya kufunga /Bei ya mwisho (Closing Price)

Hii ni bei ya mwisho kwa siku ambapo amana maalum iliuzwa.

Hatifungani zinazoweza kubadilishwa (Convertible Bond)

Ni hati fungani ambayo inaweza kubadilishwa chini ya nasharti yaliyowekwa kwa idadi fulani ya hisa za kawaida.

Muundo wa mtaji (Capital Structure)

Hizi ni sehemu mbalimbali za mtaji wa kampuni; kama dhamana ya mkopo, hisa za kawaida, hisa pendeleo na kadhalika.

Mpango wa pamoja wa uwekezaji (Collective Investment Schemes-CIS)

Hizi ni fedha zinazosimamiwa kwa niaba ya wawekezaji na mtaalamu wa maswala ya kifedha anayenunua hisa, hatifungani au amana nyingine kulingana na malemgo maalum ya uwekezaji yaliyowekwa na mpango husika. Mpango huo huchukua mielekeo hii:

(a) Hazina ya pamoja (Mutual fund): kampuni ya umma au kutoka nje iliyobuniwa kwa lengo la kusimamia amana au rasilimali nyingine za kifedha. Kampuni hukubali fedha kutoka kwa wawekezaji na hutumia hazina hiyo ili kusimamia uwekezaji huo. Kampuni hutoa hisa, ambazo huwakilisha hisa zote na hutolewa kwa wawekezaji. Hazina ya pamoja aidha huwa ni hazina wazi au hazina funge.

(i) Hazina wazi (Open-end funds) – hii ni hazina ambayo huwa tayari kununua upya hisa kutoka kwa wenye hisa katika kiwango chochote na wakati wowote mwenye hisa anataka kufanya hivyo. Pia wanauza hisa kwa kiwango chochote kwa wawekezaji wakati wowote kutegemea wawekezaji.

(ii) Hazina funge (Closed-end funds) – hii ni hazina ambayo hutoa idadi maalum ya hisa na haiwezi kununua upya kutoka kwa wenyewe wakati wanapoamua kuziuza. Sheria inasema kuwa hazina funge ziorodheshwe katika soko la hisa ili kutoa pesa taslimu kwa wenye hisa. Hisa hizi huuzwa kwa bei inayotegemea hali ya soko wakati husika.

(b) Fedha maalum (Unit trust) – Hizi ni hazina za uwekezaji zinazoleta pamoja fedha kutoka kwa wawekezaji wadogowadogo kwa viwango fulani. Fedha maalum hujumuisha stakabadhi inayojulikana kama hati aminifu na inasimamiwa na wataalamu wa maswala ya soko la hisa.

Usimamizi wa shirika (Corporate Governance)

Usimamizi wa shirika ni namna ambavyo mamlaka na uwezo wa shirika hudhihirika katika usimamizi wa rasilimali za shirika kwa lengo la kuendelea kuwepo na wenye hisa pamoja na kuwa na ongezeko katika muktadha wa maono ya shirika.

Mtaalam wa kutathmini deni (Credit Rating Agency)

Huyu ni mtaalam ambaye wajibu wake ni kutoa maoni yasiyo na upendeleo kuhusu uwezo wa mtoaji wa ala ya deni, na uwezo wake wa kutimiza masharti yake kwa wakati ufaao kwa muda wa ala hiyo ya kifedha kulingana na vigezo vya dhima ikiwemo uwezo wa mtoaji kuzalisha mapato siku za usoni.

Yote pamoja (Cum-All)

Istilahi hii humaanisha amana ina haki ya mgao, nyongeza, na kadharika. Mnunuzi wa amana ana haki kupata sio tuu hisa bali pia mgao au nyongeza na haki nyingine yoyote iliyotangazwa ambao haijalipwa bado.

Aliye haki ya mgao (Cum-Dividend)

Istilahi hii humaanisha amana ina haki ya mgao. Mnunuzi wa amana ana haki kupata sio tuu hisa bali pia mgao uliyotangazwa ambao haijalipwa bado.

Mhifadhi (Custodian)

Kampuni iliyoidhinishwa kuweka fedha, amana, ala za kifedha au stakabadhi za hatimiliki za rasilimali zilizosajiliwa kwa jina la mpango wa pamoja wa uwekezaji, wawekezaji wa humu nchini wawekezaji wa eneo la Afrika Mashirika, au wawekezaji wa kigeni. Kila mshauri wa uwekezaji na meneja wa hazina anayesimamia hazina humteua mhifadhi wa rasilimali za hazina.

Hazina ya mkopo (Debenture Stocks)

Stakabadhi ya mkopo ni hati inayothibitisha kuwa kampuni imekopa. Hati hizo zinaweza kutolewa kusimamia rasilimali maalum ya kampuni. Hata hivyo, hati hizo zinaweza kubadilishwa na amana za hisa za kawaida za kampuni iwapo mwenyewe atataka kufanya hivyo. Riba kwa hati hizo hulipwa tarehe fulani na kapuni iwe imepata faida ya kutosha au la.

Amana zizizokuwa na thamana (Dematerialized Securities)

Hii ni amana za kampuni ambazopo cheti chake hakitambulikani tena wala accounti deo hutambulikana.

Mapato yaliyopungua kwa hisa (Diluted Earnings Per Share)

Hii thamani ya kifedha ya faida baada ya kutozwa ushuru kwa kila hisa ya kawaida.

Mgao (Dividends)

Hii ni sehemu ya faida ya kampuni ambayo hugawiwa wenye hisa kama pesa taslimu baada ya kutolewa na kuadhinishwa katika mkutano wa kila mwaka. Idadi ya faida ambayo haijagawa hubakia kama akiba ya kampuni.

Mgao kwa kila hisa (Dividend Per Share)

Ni jumla ya migao iliyolipwa kugawa kwa idadi ya jumla ya hisa zilizozotolewa na kulipiwa kikamilifu. Kwa hivyo ni idadi ya mgao ulilolipwa kwa kila hisa.

Mapato ya mgao (Dividend Yield)

Ni mapato kwa kilashilingi iliyoekezwa katika amana – na mara nyingi hutolewa kama asilimia ya bei iliyo kwenye soko kwa kila hisa.

Jumla ya mgao (Dividend Cover)

Hii ni idadi ya mara kadha ya faida ya kampuni ikijumulisha malipo ya mgao na huhesabiwa kama mgao wa faida baada ya kutozwaushuru na migao kutangazwa. Jumla ya mgao inaweza pia kupatikana kwa mnunuzi kugawa mapato kwa kila hisa kwa kila mgao kwa kila hisa.

Mapato kwa kila hisa (Earnings Per Share-EPS)

Hii ni thamani ya kifedha ya faida baada ya ushuru kutozwa kwa kila hisa ya kawaida inayopatikana kwa kugawa mapato baada ya ushuru na idadi ya hisa za kawaida zilizosajiliwa. Hiki ni kipimo kinachoonyesha kuwa kampuni inapata faida.

Amana zilizo sawa (Eligible Securities)

Ni amana ambayo imepitishwa na soko la amana kutumiwa na kitengo kikuu cha rubuni.

Ufadhili wa hisa (Equity Financing)

Ufadhili wa hisa ni pesa zinazopatikana kutoka kwa masoko ya mitaji kwa kutoa amana kama vile hisa. Ni ufadhili wa shughuli za kampuni kwa kutumia pesa za wanahisa.

Hazina za uwekezaji za pamoja (ESOP- Unit Trust)

Mipango ya umiliki wa hisa kwa msajiliwa. Huu ni mpango wa pamoja wa uwekezaji kwa njia ya dhamana. ESOP ni mpango ambao hutumiwa na waanjiri kuwaruhusu waanjiriwa wa kampuni zilizoithinishwa katika soko la hisa kununua idadi fulani ya hisa katika kampuni zao kwa bei fulani. Bei katika mpango huu inaweza kuwa chini ya bei iliyo ya soko

Mgao wa hapo nyuma (Ex-Dividend)

Istilahi hii humaanisha amana haina haki ya mgao. Mnunuzi wa amana hana haki kupata mgao uliyotangazwa ambao haijalipwa bado.

Yote hapo nyuma (Ex-All)

Istilahi hii humaanisha amana haina haki ya mgao, nyongeza, na kadharika. Mnunuzi wa amana hana haki kupata mgao au nyongeza na haki nyingine yoyote ambayo imetangazwa lakini bado haijalipwa bado.

Taarifa ya kifedha (Financial Instruments)

Ni mkataba unaoibua rasilimali za kifedha za kampuni, na madeni ya kampuni kutoka kwa kampuni nyingine.

Masoko ya kifedha (Financial Markets)

Haya ni masoko ya kifedha hujumuisha masoko ya pesa nay ale ya na mitaji ambayo huunda mfumo wa kifedha. Soko la pesa ni mipango ya mda mfupi ya masoko ya kifedha kiwango cha chini ya mwaka mmoja. ilhali masoko ya mitaji ni mipango ya muda mrefu (kiwango cha juu ya mwaka mmoja).

Mpango wa kifedha (Financial Plan)

Huu ni utaritibu ambapo mwekezaji hulinganisha hali yake ya kifedha na malengo yake ya uwekezaji katika mazingira ya kifedha yanayobadilika.

Mkataba wa siku zijazo (Futures Contract)

Ni mkataba wa kununua au kuuza bidhaa au ala ya kifedha tarehe fulani siku zijazo kwa bei inayoaganawa na wahusika wakati mkataba unavyoadikwa .

Hatifungani yenye hakikisho (Guaranteed Bond)

Hii ni hati fungani yenye hakikisho ya kulipwa na Kapuni nyingine, (mara nyingi) anayejulikana zaidi na mwenye uwezo mkubwa kifedha kuliko mtoaji hatifungani kama kampuni inayohusika ikishidwa kulipa.

Kinga (Hedge)

Ni mkakati wa kuondoa au kupunguza dhima katika uwekezaji.

Mkataba wa hatifungani (Indenture)

Huu ni mkataba unaosimamia suala la hatifungani. Mtoaji wa hatifungani na mdhamini anayewakilisha wenye hatifungani hutia sahihi mkataba na kuweka wazi wajibu na haki za mtoaji, mdhamini, na wenye hatifungani pamoja na masharti

yanayohusu uhalali.

Kielezo (Index)

Huu ni utaratibu wa hesabu unaopima mabadiliko katika uchumi au masoko ya kifedha. Kielezo hupima kupanda na kushuka kwa bei ya bidhaa na huduma, hisa, hatifungani na bidhaa za soko.

Utoaji wa hisa kwa umma wa kwanza (Initial Public Offering-IPO)

IPO ni toleo kwa umma kununua amana zilizotolewa kwa mara ya kwanza.

Mwekezaji (Investor)

Ni mtu au taasisi inayotumia akiba yake au mkopo kununua amana.

Hazina ya kufidia mwekezaji (Investor Compensation Fund)

Hii ni hazina ya kufidia wawekezaji ambao hupata hasara kutokana na kushindwa kwa dalali au mfanyi biashara wa hisa kutimiza wajibu wake wa kimkataba.

Uwekezaji (Investment)

Uwekezaji ni utumizi wa fedha kwa ajili ya uzalishaji katika masoko ya kifedha.

Mshauri wa uwekezaji (Investment Adviser)

Watu au kampuni iliosajiliwa na CMA ambayo hujihusisha na biashara ya kuwashauri wateja wao kuhusu thamani ya amana zao na iwapo ni vyema kewekeza, kununua au kuuza amana. Washauri hawa pia hufanya uchunguzi kuhusu amana na huweza kusimamia uwekezaji chini ya mkataba na wawekezaji.

Benki ya uwekezaji (Investment Banks)

Hi ni taasisi isiyochukua pesa za dipositi kama banki za kawaida, ambayo hushauri kuhusu utolewaji wa amana kwa umma au sehemu ya umma, marekebisho ya taasisi za kifedha, uunganishi wa kampuni, usimamizi mpya wa kampuni, ubinafsishaji wa kampuni na utolewaji wa amana. Pia hi banki hujihusisha na biashara ya udalali, umeneja na uwekezaji, usimamizi wa hazina na utoaji wa huduma za usimamizi.

Mtoaji (Issuer)

Neno "mtoaji"hutumiwa kurejelea kampuni au taasisi yoyote ya kisheria ambayo amana zake zinatumiwa maombi ili kuorodhesha nchini Kenya au zimeorodheshwa tayari.

Mtaji wa hisa uliotolewa (Issued Share Capital)

Hiki ni kiwango cha mtaji ambacho kimetolewa na kulipiwa kutoka kwa mtaji wa hisa ulioidhinishwa na kampuni.

Siku ya mwisho ya kusajiliwa katika kampuni au siku ya kufunga vitabu vya kampuni (Last Day To Register Or Books Closing Date)

Hii ni siku ambapo amana hufikia ofisi za kampuni ili ziweze kufuzu kwa kupata mgao au nyongeza na haki nyingine yoyote ambayo imetangazwa lakini bado haijalipwa bado

Agizo la kiwango cha chini (Limit Order)

Ni agizo linalotolewa na mwekezaji kwa dalali likieleza kiwango cha chini cha bei ambazo hisa inaweza kuuzwa au kununuliwa.

Thamani ya kampuni katika soko(Market Capitalization)

Hiki ni kiwango cha kukadiria cha thamani ya kampuni kinachopatikana kwa kuzidishia bei ya sasa ya soko kwa idadi ya hisa zilizotolewa na kulipiwa wakati wa kipindi maalum.

Bei ya soko (Market Price)

Hii ni bei ya hisa inayotawala katika soko la hisa wakati wowote ule.

Tarehe ya kupevuka (Maturity Date)

Hii ni tarehe iliyowekwa kwenye, hatifungani au ushahidi wowote wa kideni kuonyesha tarehe amana itahitaji kulipwa na kusitishwa. Tarehe ya kupevuka hutegemea masharti ya deni.

Muungano wa kampuni (Merger)

Inamaanisa kuunganisha kampuni mbili au zaidi kuwa moja ambapo wenye hisa huendelea kuwa na mamlaka, na haki ya faida katika kampuni mpya.

Kiasi witiri (Odd Lots)

Hiki ni ya kiwango cha chini kuliko idadi inayoweza kuuzwa moja kwa moja katika soko kuu..

Toleo (Offer)

Ni kiwango cha chini kabisa cha bei ambacho dalali au mfanyibiashara anaweza kuuza amana kwa niaba ya mteja.

Kilio cha wazi (Open Outcry)

Ni mfumo wa ufanyibiashara katika soko la hisa ambapo madalali hutangaza kwa sauti ya juu bei za amana kwahisani ya wateja wao.

Ufanyibiashara kwenye kaunta (Over-The-Counter Trading-OTC)

Haya ni matoleo yanayofanyiwa biashara ya amana kwenye soko kupashana habari kwa njia isio ya kirasmi. Pia hujulikana kama kufanya biashara nje ya soko maalum.

Mtaji uliolipiwa (Paid Up Capital)

Hiki ni kiwango cha mtaji kinacholipwa na wenyehisa wa kampuni na ni jumla ya hisa zilizotolewa kuzidisha thamani ya kila hisa.

Thamani ya amana (Par Value)

Ni thamani ya amana inayoonyesha kwenye amana husika. Kwa amana iliyofanyiwa biashara, thamani hutumiwa kwa minajili ya uwekaji hesabu za kifedha tu.

Orodhaamana (Portifolio)

Ni mkusanyiko wa dhamana mbalimbali zinazochukuliwa na mwekezaji au taasisi au kundi la amana ambapo umma hualikwa kununua hisa. Orodhafedha inaweza kujumuisha hisa zilizopendelewa, hisa za kawaida na hatifungani za kampuni mbalimbali.

Kikomo cha hisa cha kawaida (Potential Ordinary Share)

Ni mkataba wa kifedha unaompa mnunuzi haki ya kununua hisa za kawaida. Hiari ni mfano wa ala za kifedha zinazompa mnunuzi haki ya kununua hisa za kawaida.

Ubinafsishaji (Privatization)

Hiki ni kitendo cha kuhamisha rasilimali za serikali hadi mkononi mwa watu binafsi au umma, kwa kutoa toleo kwa umma, zabuni au muktaba wa kibinafsi. Kitendo hiki pia huitwa upunguzaji rasilimali kwani serikali husambaza uwekezaji wake kwa kampuni za ubinafsi.

Mwakilishi (Proxy)

Ni kuidhinishwa na mwenye hisa wa kampuni kuhamisha haki yake ya kupiga kura kwa mtu mwingine kupitia maagizo yaliyoandikwa.

Kielelezo (Prospectus)

Ni stakabadhi, arifa, matangazo au njia nyingine yoyote ya mwaliko kwa umma kuwaalika wanunue hisa au amana za kampuni. Hiki kielelezo hujumusiha masharti, mtaji unaotakikana, malengo au mipango ya matumizi ya pesa zitakazopatikana kutokana na toleo, historia ya kifedha ya kampuni, pamoja na maelezo mengine yanayoweza kumsaidia mtu kuamua iwapo uwekezaji huo utamfaa au la. Pia huitwa taarifa ya toleo.

Toleo kwa umma (Public Offer)

Ni toleo linalotolewa na kampuni kwa umma ili kununua hisa mpya au zilizopo zinazotolewa kuuzwa kwa umma kama ilivyo katika mpango wa ubinafsishaji.

Thamani ya kiasili ya hisa (Par Value-Nominal)

Ni thamani inayopewa hisa zinazotolewa hazina uhusiano wowote na thamani ya kawaida kwenye soko (market price).

Kima cha mapato cha bei (Price Earning Ratio-P/E)

Hii ni idadi ya mara kadha inayomchukua mwenye hisa kupata uwekezaji wake katika hisa.

Soko la msingi (Primary Market)

Hili ni toleo la awali la amana kabla ya kujumuishwa katika soko la hisa ambapo amana hufanyiwa biashara

Toleo la kibinafsi (Private Placement)

Huu ni uuzaji wa amana moja kwa mataasissi kaama vile benki, kampuni za bima, Mpango ya pamoja wa uwekezaji na wakfu.

Uuzaji wa papo hapo (Prompts Lots)

Huu ni uuzaji wa amana, ambao sharti uwasilishwe kabla saa tisa siku iyo hiyo na pande zote mbili.

Kampuni ya umma (Public Company)

Hii ni kampuni iliyoundwa kwa mujibu wa sheria na si kampuni ya kibinafsi. Kampuni ya umma iliyo orodheshwa haiwezi kuwa na vikwazo vyovyote katika ubadilishaji wa hisa zake.

Bei inayotangazwa kwenye soko (Quotation)

Hii ni bei ambayo amana inayotangazwa katika soko la hisa.hii bei hutofautiana kutoka wakati mmoja hadi mwingine kutegemea utashi na ugavi wa amana.

Usajili (Regisration)

Usajili ni hali ya kuingiza majina na anwani za wenyehisa wote kwenye rejista ya kampuni. Baadaye mwenyehisa huwa na haki ya umiliki na ile ya kupokea ripoti, arifa na mgao unaotolewa na kampuni.

Toleo jipya kwa wenye hisa waliopo kwa kampuni (Rights Issue)

Hii ni toleo kwa wenyehisa waliopo kununua hisa mpya, wakati mwingi, kwa bei maalum inayowapendelea kwa mujibu wa hisa zao katika kampuni.

Akiba ya mapato (Revenue Reserves)

Hii ni sehemu ya mapato yaliyobaki kwa kampuni ambayo hugawiwa wenyehisa kama bonasi au mgao siku za usoni au hutumiwa kwa upanuzi wa kampuni.

Mapato yanayobakizwa (Retained Earnings)

Sehemu ya pato halisi la kampuni ambalo haligawanywi kama faida kwa wenye hisa, bali hubakia kwa ajili ya upanuzi wa kampuni.

Skiripi (Scrip)

Neno hili humaanisha vyeti vya hisa.

Skiripi au mgao wa hisa (Scrip Or Stock Dividend)

Hii ni hisa ambayo hutolewa kwa wenyehisa waliopo badala ya mgao.

Soko la pili/ubandilizanaji (Secondary Market)

Hii ni soko ambapo amana hufanyiwa biashara baada ya toleo la awali.

Amana (Securities)

Hizi ni ala za kifedha au stakabadhi za kifedha zinazoonyesha umiliki wa kampuni au umiliki wa hatifungani za kampuni.

Kipindi cha malipo (Settlement Period)

Huu ni muda uliotengwa kwa mujibu wa tarehe ya ufanyajibiashara ambapo madalali wanahitajika kutoa amana au kulipia amana walizo fanyia biashara kupitia soko la hisa.

Hisa (Shares)

Hisa humaanisha umiliki wa kampuni na hugawa katika aina mbalimbali kama:

Hisa za kawaida (Ordinary Shares)˜ hizi ni hisa zinazompa mweyhisa umiliki wa kiasi wa kampuni kulingana na idadi ya hisa alizonazo na kumwezesha kupata mgao.

Hisa pendelezi (Preference Shares)˜ hizi ni hisa zenye kiwango maalum cha mgao cheenye uwezo zaidi ya hisa za kawaida katika mgao wa faida kutokana na faida ya mwaka,

Hisa zinazoweza kununuliwa (Redeemable Shares)˜ hizi ni hisa zinazoweza kununuliwa kutoka kwa wenye hisa na kampuni wanayomiliki kwa tarehe na bei maalum au katika masharti fulani kwa uamuzi wa halmashauri hiyo kampuni.

˜Hisa pendelezi zinazoweza kubadilishwa (Convertible Preference Shares) ˜hizi ni hisa pendelezi zinazoweza kubadilishwa chini ya masharti kuwa idadi fulani ya hisa za kawaida au kwa kiasi cha hatifungani fulani za mtoaji.

Cheti cha hisa (Share Certificate)

Hii ni stakabadhi inayoonyesha umiliki wa hisa. Inaweza kutumiwa kama dhamana ya mkopo katika kupata mkopo.

Msambao (Spread)

Tofauti kati ya bei inayonunuliwa amana na bei iliyotolewa.

Dalali anayedhamini (Sponsoring Broker)

Huyu ni dalali anayeteuliwa na mtoaji hisa anayetaka kuorodheshwa ili eendeshe mawasiliyano ya kampuni, CMA na soko la hisa katika utaratibu wa kuhakikisha toleo limefaulu.

Kielelezo cha soko la mtaji (Stock Market Index)

Kielezo ni kipimo cha utendaji wa soko la hisa. Kielezo kinaweza kutumiwa kama kipimo na hali (kupanda au kushuka) ya bei katika soko la hisa. Kupanda kwa kielezo huonyesha kuwa hisa zinapanda thamani. Kielelezo ni njia ya kupima utendaji wa soko.

Dalali wa mtaji (Stockbroker)

Huyu ni mtaalam wa soko anayenunua na kuuza amana kwa niaba ya wateja katika soko la hisa naye hulipwa ada ya udalali.

Mfanyibiashara wa mtaji (Stock Dealer)

Huyu ni mtu anayefanya biashara ya kununua, kuuza amana katika akaunti yake wala si kwa niaba ya wateja. Faida yake hupatikana pale bei ya amana inapopanda.

Soko la hisa (Stock Exchange)

Hili ni soko linalopewa kibali cha kuuza na kununua amana zilizoorodheshwa (hisa, mtaji na hatifungani). Katika soko hili watu binafsi na kampuni wanaweza kuunua hisa za kampuni kupitia madalali walioidhinishwa na wafanyibiashara hivyo basi kuwa wamiliki wa hizi kampuni au wamiliki wa hatfungani za hizi kampuni. Kwa sasa, ni Soko la Hisa la Nairobi tu ambalo limepewa leseni ya kubadilisha amana nchini Kenya.

Kiwango cha biashara (Trade Volume)

Jumla ya idadi ya hisa zilizofanyiwa biashara katika amana moja wakati wa kipindi fulani. Pia ni jumla ya idadi ya hisa zilizofanyiwa biashara katika soko la hisa wakati wa kipindi maalum.

Uwanjaya w a biashara (Trading Floor)

Eneo katika soko la hisa ambapo biashara hufanyika.

Hawala za serikali (Treasury Bill)

Amana za muda mfupi wa mwaka mmoja au chini zilizoidhiinishwa na serikali ya Kenya ambazo huweza kulipwa anayezimiliki. Hawala hizi huipa serikali uwezo wa muda mfupi wa kukopa na huuzwa kwa misingi ya asilimia fulani ili mapato yawe ni tofauti baina ya bei ya ununuzi na thamani yake ya sasa.

Hatifungani za serikali (Treasury Bond)

Hii ni amana yenye riba iliyowekwa inayotolewa na serikali kama njia ya muda mrefu ya kujipatia pesa na hutolewa ikawa na muda wa zaidi ya mwaka mmoja.

Udhamini (Trust)

Mpango wa kifedha ambapo mtu (anayedhamini) huchukua usimamizi wa mali ya mtu au taasisi (mdhamini) kwa manufaa ya watakaonufaika.

Mdhamini (Trustee)

Mtu au shirika ambalo husimamia na huwekeza rasilimali kwa manufaa ya mwingine. Mdhamini anashurutishwa kisheria kufanya maamuzi yenye kujali maslahi ya anayedhaminiwa na anaweza kushtakiwa iwapo hatekelezi majukumu haya. Mdhamini ana haki ya kulipwa kwa huduma anayotoa iwapo imeelezwa kwenye hati ya udhamini. Katika suala la soko la hatifungani, mdhamini husimamia toleo la hatifungani kwa anayekopa na uhakikisho kwa mtoaji anatimiza masharti yote yanayohusika ya ukopaji. Kwa upande wa hati za udhamini, mdhamini huwekeza pesa kwa uwekezaji ambao unakaguliwa na serikali.

Hati ya udhamini (Trust Deed)

Hii ni hati ya udhamini ambayo hueleza masharti ya usimamizi wa udhamini

Washauri wa hisa (Underwriters)

Hawa ni wataalam na washauri ambao huchukua dhima ya ufanisi au kutofaulu kwa hisa zilizotolewa kwa umma.

Hazina ya mtaji (Venture Capital Fund)

Kampuni iliyoundwa kwa minajili ya kutoa fedha au mtaji wa kina kwa biashara ndogondogo ambazo ni mpya na zina matumaini ya kukua

Waranti (Warrant)

Ni ala ya serikali ambayo humpa mwenye hisa haki sio ulazima wa kutuma maombi ya hisa mpya za kawaida kwa bei iliyowekwa kwa muda fulani. Waranti hazina thamani yoyote baada ya kumalizika kwa kipindi kilichotengwa.

Disclaimer

Maelezo yaliotolewa kwenye mwongozo huu yanatolewa kama yalivyo bila uhakiki wa aina yoyote.
Capital markets Authority haitoi uthibitisho wa usahihi na ukamilifu kwenye mwongozo hu

Mwongo huu umetayarishwa na Capital Markets Authotrity kwa udhamini wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP).

CAPITAL
MARKETS AUTHORITY

© CMA 2006.